# JARIBIO LA MTIHANI
## DARASA LA NANE - 2020
## KISWAHILI:LUGHA (73314403)

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina Maswali 50. **Muda: Saa moja Dak. 40**
2. Hakikisha umeandika: (i) **NAMBA YAKO YA MTIHANI** (ii) **JINA LAKO** (iii) **JINA LA SHULE YAKO**
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

***Jaza nafasi 1 - 15 kwa vihasho sahihi.***

Utunzaji bora wa mazingira ni jambo __1__ katika maisha ya __2__. Hii ni __3__ kila kiumbe hutegemea mazingira kuishi __4__ kabisa sisi __5__ tutaangamia.

Sehemu muhimu ya mazingira ni msitu. Misitu __6__ manufaa __7__. Kwanza misitu __8__ mawingu ya mvua. Mvua __9__ huwasaidia wakulima kupata mazao ya kuyajaza __10__ yao. Misitu pia ni __11__ ya wanyama. Wanyama hawa huwavutia __12__ ambao hutuletea fedha za kigeni.

Misitu pia huwa vianzio au chemichemi za __13__. Nayo maji ya mito hiyo hutumiwa kunyunyuzia mashamba. Kwenye misitu tunapata __14__ ambayo hutupa matunda. Aidha __15__ tunazopata sebuleni hutokana na miti.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. jizuri | B. nzuri | C. lizuri | D. zuri |
| 2. | A. watu nyote | B. watu kamili | C. viumbe vyote | D. viumbe wote |
| 3. | A. kwa sababu | B. kwa minajili | C. kwa kua | D. kwa kawaida |
| 4. | A. yakiaribishwa | B. zikiharibiwa | C. yakiharibiwa | D. ikiharibiwa |
| 5. | A. wote | B. nyote | C. zote | D. sote |
| 6. | A. yana | B. ina | C. zina | D. una |
| 7. | A. mingi | B. tele | C. mwingi | D. nyingi |
| 8. | A. huvuta | B. huvuvuta | C. huvutia | D. hufuta |
| 9. | A. jikinyesha | B. yakinyesha | C. ikinyesha | D. likinyesha |
| 10. | A. maghala | B. stoo | C. vyumba | D. matumbo |
| 11. | A. makaazi | B. makazi | C. nyumba | D. mbuga |
| 12. | A. watu | B. wakimbizi | C. wananchi | D. watalii |
| 13. | A. maji | B. mvua | C. mito | D. miti |
| 14. | A. matunda | B. mitunda | C. mti | D. kuni |
| 15. | A. samani | B. vyombo | C. viti | D. zamani |

***Kutoka swali la 16 - 30 chagua jibu sahihi.***

16. Katika nyumba yetu tuna vijiko vya _____ chakula.
    A. kukula B. kukulia
    C. kula D. kulia
17. ***Chagua wingi wa sentensi hii:***
    Nitaifagia nyumba yangu leo.
    A. Watafagia nyumba yangu leo.
    B. Tutazifagia nyumba yangu leo.
    C. Tutafagia, nyumba yetu leo.
    D. Tutazifagia nyumba zetu leo.
18. 9,500,894 kwa maneno ni
    A. Milioni tisa, laki tano, mia, nane tisini na nne
    B. Milioni tisa, elfu mia tano, mia nane tisitini
    C. Milioni tisa, elfu mia tani, mia nane tisini na nane.
    D. Milioni sita, laki tano, mia nane tisini na nne
19. Wakati kuanzia saa sita mchana hadi saa tisa huitwa
    A. alasiri B. adhuhuri
    C. majogoo D. machweo
20. Kifaa ambacho hutumika kufunikia chakula huitwa
    A. upawa B. mkungu
    C. kawa D. ungo
21. ***Jaza pengo:***
    Nilisikia habari hizo ______ redio.
    A. kwenye B. katika
    C. kwa D. ndani ya

22. ***Kanusha***

Njoo na mle.

A. Njooni na msile  B. Msikuje na msikule
C. Msije na msile  D. msije wala msile

23. Chagua kauli sanifu kisarufi.

A. Chakula kimo mfukoni mwangu.
B. Chakula kimo mfukoni wangu.
C. Chakula kiko kwa mfuko wangu.
D. Chakula kipo mfukoni pangu

24. Tunasema robota la pamba. Shehena ni ya

A. udongo  B. magari
C. mizigo  D. sahani

25. ***Sentensi ifuatayo ipo katika wakati gani?***

Chakula hupikwa kitaalamu na mama.

A tegemezi  B. mazoea
C. uliopita  D. timilifu

26. ***Kamilisha methali:***

Kosa moja haliachishi ______

A. mke  B. mtoto
C. mhalifu  D. mwingi

27. Maamkizi ya asubuhi ni ______

A. alamsiki  B. masalkheri
C. sabalkheri  D. binuru

28. Chagua sentensi yenye **ki** ya kuonyesha masharti.

A. Kiatu kile kitaoshwa.
B. Mwanafunzi yule alilia kitoto.
C. Akija kule atanipata.
D. Kigombe hiki kitauzwa.

29. Mwindaji haramu katika mbuga za wanyama huitwa

A. jangili  B. jambazi
C. msasi  D. msusi

30. Akisami $^7/_9$ huitwa

A. tusui saba
B. sudusi saba
C. subui tisa
D. tusui tisa

***Soma makala haya kisha ujibu maswali 31 - 40.***

Iwapo kuna uele unaoogofya zaidi, sharti uwe UKIMWI. Umepachikwa majina tofauti na watu tofauti yote yakiashiria udhalimu wake. Kunao walio na imani potovu kuwa si ugonjwa bali ni uchawi, eti wamerogwa. Ushirikina huu umeathiri hata waliosoma. Do! Ingawa wengi wana mwao kuuhusu, wengine ni waledi **wao** kabisa.

Uvumi unaposambazwa au inapobainika bayana kuwa mja ameambukizwa, wengi humwambaa. Wengine humsema kutwa kucha huku idadi ndogo ikimhurumia. Wagonjwa wengi hawafi kutokana na makali ya virusi vinavyosababisha UKIMWI ila kwa **unyanyapaa** unaofuata kutoka kwa aila na jamii.

Je, ushawahi kuwazia kuhusu maambukizi ya ugonjwa wenyewe? Inafahamika vyema maambukizi yaliyo katika mstari wa mbele ni kutokana na mapenzi ya kiholela. Wenye macho ya nje, viruka - njia na viruka - mito wengi wamejiendea jongomeo kupitia njia hii. Angalau afueni imepatikana baada ya kampeni kabambe kuhusu uenezaji wa UKIMWI. Sampuli ya moto jangwani. Aidha, tarakimu za wahasiriwa na wafu, zilipoanza kutangazwa hadharani, asilimia kubwa ya watu imebadilisha nyendo zao. Hili ni jambo la busara linalostahili kuigwa na wote.

Ikumbukwe kuwa kunao wanaoambukizwa bila hiari. Kundi hili husahaulika na wengine wanaposhutumiwa, wao pia huathiriwa na kutezwa huko. Baadhi yao hujichukia kiasi cha kujitia kitanzi huku wengine wakijisononekea hadi kaburini.

Kundi hili linajumlisha vimalaika wa Mungu (wanaoambukizwa wakiwa bado tumboni mwa mama zao) na wanaobakwa na katili, watu wasio na utu.

Hali kadhalika maghulamu waweza kuambukizwa wanapopash[illegible]a tohara na ngariba wapuzi kwa kisu kimoja. Iwapo mmoja wao ana virusi, uwezekano wa maambuk[illegible]izi ni mkubwa. Isitoshe, majeruhi ajalini wanaovuja damu waweze kuambukizana. Madaktari na waug[illegible]izi wasipotumia vifaa safi waweza kueneza maambukizi. Tusisahau, waganga na waganguzi. Wawachan[illegible]o wateja wao kwa nyembe kuukuu zilizotumika mara alfeni.

Kunazo njia nyingine za kueneza maambukizi ingawa nadra mn[illegible]. Mathalani; daktari au mwuguzi kwa bahati mbaya aweze kujidunga kwa sindano aliyomdungia na nd[illegible]ge mbaya hulaumiwa kwa makosa yasiyo yao. Tusikaushe visima vyetu vya huruma madhali ukiona cha [illegible] wenzako kikinyolewa, chako kitie maji.

Madhali tiba ya uele huu bado haijapatikana, ni faradhi tutahadh[illegible]i kabla ya hatari.

Kinga ni bora kuliko tiba. Kwa wahasiriwa tubadilishe mtazamo [illegible]tu. Tuwafanyie jamala, tuwapende na kuwajumlisha katika shughuli zetu zote na kuwaona kuwa ndugu [illegible]

Heko kwa wanasayansi wanaondelea kugundua dawa za kupu[illegible]guza makali ya virusi vyenyewe. Inshallah tiba kamili huenda ikapatikana na kufuta machozi ya wana[illegible]gua.

31. Dhana tunayopata kutoka aya ya kwanza ni kuwa
   A. UKIMWI ni doto mbaya inayoogofya
   B. jamii tofauti ziemupa ugonjwa huu majina tofauti
   C. majina mengine yanayopewa UKIMWI huonyesha ubya na umabukizi wake mbaya.
   D. jamii zinaogopa ugonjwa wenyewe na kuupa majina ya kuonyesha hivyo.
32. Mtu anaposemekana kuwa na UKIMWI
   A. wengi humweonea huruma, wengine humtenga wote humsema
   B. wengi humsema, wachache humhurumia, wengine humtenga
   C. wengi humtenga, wachache humhurumia, wengine humtenga
   D. wote humwambaa, wengine humsema, wengi humhurumia.
33. Neno **wao** kama ilivyotumika katika aya ya kwanza lina maana ya
   A. wagonjwa wa UKIMWI
   B. ugonjwa wa UKIMWI
   C. weledi wa UKIMWI
   D. virusi vya UKIMWI
34. Ni kweli kusema kuwa
   A. wanaoambukizwa ni wenye macho ya nje na viruka njia
   B. watoto na wanaobakwa ndio huambikiza bila hiari tu.
   C. kunao wale huambukizwa kwa kujitakia
   D. majeruhis wote katika ajali huambukizwa
35. Baadhi ya wanaojinyonga kutokana na maradhi hushinikizwa na
   A. kudharauliwa, kulaumiwa na kutojithamini
   B. maumivu, makali kutokana na magonjwa
   C. kutojichukia, kutwezwa na kushurutiwa
   D. magonjwa mbalimbali na aibu wanayoona
36. Watu wengi wanawabagua na kuwachukia wagonjwa kwa sababu ya
   A. hawana mwao kuhusu chanzo chake
   B. kutojua kiini cha ugonjwa na mtazamo mbaya
   C. visima vyao vya huruma vimekauka
   D. ushirikina wa imani kuwa wagonjwa wamerogwa
37. Neno **unyanyapaa** kama lilivyotumika lina maana ya
   A. kumpa mgonjwa machungu kwa kichapo
   B. kutompeleka mgonjwa kutibiwa kwa kumchukia
   C. majivuo ya jamaa na jamii kwa magonjwa
   D. kudharau wengine na kujiona bora
38. Methali **'ukiona cha mwenzako chanyolewa kitie chako maji'** ina maana kuwa
   A. ugonjwa wa ukimwi huambukizwa na ndege mbaya.
   B. tutahadhari tusipatwe na ugonjwa wenyewe
   C. yeyote yule aweza kupatwa na ugonjwa huu
   D. tuwahurumie na kuwapenda wagonjwa
39. Sentensi ya mwisho ya aya ya mwisho
   A. inawafuta machozi wagonjwa
   B. inawapa wagonjwa matumaini
   C. inawapongeza watafiti
   D. inawapa wagonjwa motisha
40. Itakuwa vyema iwapo ngariba wanaotahiri wana wa kiume
   A. wataosha visu vyao vya kuwapashia tohara
   B. watatumia kisu kimoja kwa wavulana
   C. watawajibika na kutotumia kisu kimoja
   D. watatumia kisu kimoja kwa ghulamu mmoja

***Soma kifungu kifuatahco kisha ujibu maswlai 41 - 50.***

Zainabu alikiona kilichomfanya kuku kukosa meno hivi juzi juzi. Huku michirizi ya machozi ikimchirizika, na akiwa na uchungu mwingi alisikika akilia kwa kusema, "ole wangu. Majuto ni mjukuu. kama ningalijua nisingalitoa mimba hiyo sasa nimebaki na kaburi mwilini. Mungu wangu, naomba unisamehe kwa kuua kiumbe chako bila sababu yoyote.

Zainabu, msichana wa miaka kumi na minane alipata mimba hiyo akiwa kidato cha nne. Alienda kwa mganga wa kichochoroni na mganga huyo alipokuwa akitoa mimba hiyo, Fatuma alianza kuvuja damu nyingi akazirai. Mganga kuona mambo yalivyokuwa yakizidi kuwa mabaya alimwacha hapo kitandani na kutimua mbio. Kwa bahati nzuri msamaria mwema alimchukua msichana huyo hadi kituo cha matibabu alikolazwa huko kwa muda wa miezi mitatu.

Jambo la kuhuzunisha na lililomtia Zainabu hofu sana ni kujua kuwa alikuwa ameyaangamiza maisha ya kiumbe cha Mungu. Mawazo hayo yangali yanamtatiza mpaka leo na kila anapokumbuka kitendo hicho machozi kumtoka. Isitoshe daktari pia alimfahamisha kuwa katika maisha yake yote ya baadaye, hataweza kuzaa tena kwa sababu sehemu zake za uzazi hasa nyumba ya mtoto ilikuwa imeharibika kabisa.

Uharibifu huo ulikuwa umesababishwa na vifaa ambavyo mganga huyo bandia alikuwa akivitumia kwa utoaji mimba.

41. Maana ya methali **"majuto ni mjukuu"** n

A. majuto ni mtoto wa mwanawe babu
B. utajuta ukimchokoza mwenzako
C. ukifanya matendo mabaya au kukosa utajuta baadaye
D. ukienda kwa mwendo wa kufanya jambo kwa wakati wake, utasikika polepole ukijuta.

42. Ni nini maana a michirizi ya machozi?

A. Machozi yalimlengalenga machoni
B. Machozi yalimjaa machoni
C. Kulia bila kutoa sauti ya kwi kwi kwi
D. Njia nyembamba ya machozi

43. Zainabu alijiunga na shule ya upili akiwa na umri wa miaka

A. kumi na mitano
B. kumi na sita
C. kumi na minane
D. kumi na minne

44. Kwa nini mganga alitimua mbio?

A. Kwa sababu Zainabu alikuwa amefariki
B. Aliogopa damu nyingi iliyoendelea kuvuja
C. Alikuwa ameangamiza kiumbe cha Mungu
D. Alikuwa na hofu Zainabu alipotokwa na damu nyingi kisha akazirai

45. Kulingana na habari hii, baada ya kutoa mimba Zainabu alithibitishiwa kuwa

A. muuaji
B. tasa
C. mganga
D. kahaba

46. Ni mawazo yapi ambayo yangali yanamtatiza Zainabu mpaka leo?

A. Kuangamiza kiumbe cha Mwenyezi Mungu
B. Fikira kwamba hatazaa tena
C. Kuharibiwa maisha na mpenziwe
D. Kutokwa na damu nyingi

47. Ni msemo upi ufaao kutumiwa badala ya **'kutimua mbio'**?

A. Kwenda kukuru kakara
B. Kutimua timu timu
C. Kwenda shoti
D. Kwenda pukutu! pu

48. Maana ya neno kuzirai ni

A. kufariki
B. kupotewa na fahamu
C. kushikwa na kisunzi
D. kulala

49. Neno jingine sawa na **'kutoa mimba'** ni

A. kuavya
B. tasa
C. kuua
D. kunyonga

50. Nyumba ya mtoto ilikuwa imeharibika kabisa. Nyumba inayorejerewa kwenye kifungu ni

A. nyumba anamolala mtoto
B. chupa
C. mahali mtoto anapitia anapozaliwa
D. mahali mtoto anaishi akishazaliwa